Huduma Ya Upatanishi
(The Ministry of Reconciliation)

Na

Ellis P. Forsman

Huduma Ya Upatanishi

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Huduma Ya Upatanishi

2 Wakor. 5:18-21

Wazo muhimu na ambalo ni la msingi kwa ajili ya injili ya Kristo ni ile ya "*upatanisho*"

2 Wakor. 5: 18-20, *"Lakini vyote pia viatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao, naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu. Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."*

Paulo anaeleza juu ya somo hili. Anaeleza jinsi a livyo na upatanisho kati ya Mungu na mwanadamu. Anaeleza sehemu aliyofanya kwa kile anachokiita "*huduma ya upatanishi*".

Kuna maswali kadhaa ambayo ningependa kuwakilisha katika somo hili...

- Kihalisi upatanishi huu una asili gani kati ya Mungu na wanadamu?
- Tunaweza kufanya upande gani katika injili ya Kristo kama "*huduma ya upatanishi*"?

Ni muhimu kufahamu kwanza maana ya neno "*upatanishi*" na umaana wake jinsi linavyo husiana na Mungu na wanadamu.

Njia Ya Upatanishi

Kufafanua upatanishi

Tafsiri Vine juu ya "upatanisho" (Kiyunani, katallasso). "hakika inaelekea kubadilika, kubadilishwa (hasa pesa)". Vile vile, watu, kubadilika kutoka katika uadui hadi katika urafiki, kupatanisha".

Binadamu amejitenga yeye binafsi na Mungu. Kuna uadui kati ya Mungu na wanadamu (kwa sababu ya dhambi ya mwanadamu. Isaya 59:1-2, *"Tazama mkono wa BWANA haukupungua hata asiweze kuokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia.*

Na, injili inatangaza jinsi MUNGU alivyochukua uamuzi wa kupatanisha mwanadamu arudi kwake. Hata hivyo, Mungu hapatanishwi ili amrudie mwanadamu, kana kwamba kwa sehemu angeweza kulaumu kwa ajili ya uadui. Badala yake, mwanadamu anapatanishwa ili amrudie Mungu, kwa maana mwanadamu ndiye anayekwenda mbali na Mungu!

Wakati watu wanapohitaji kupatanishwa mmoja dhidi ya mwingine, kwa kawaida inahusisha hali ambayo kosa linaegemea pande zote mbili kwa kiwango fulani. Lakini siyo ivyo kati ya Mungu na mwanadamu; mwanadamu amemuacha Mungu, na ni juu ya mwanadamu kupatanishwa ili amrudie Mungu, na siyo Mungu amrudie mwanadamu!

Jinsi upatanishi unavyofanywa ili iwezekane

Inawezekana kwa sababu Mungu ameichukuwa kwanza! Inawezekana kupitia Yesu Kristo, sabamba na kifo chake kwa ajili ya dhambi zetu! Zingatia misitari hii inayofundisha upatanishi unakuja kupitia Yesu.

- 2 Wakor. 5:18, *"Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho."*
- Wakol. 1:19-20, *"Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake, kwa yeye ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni."*

Kumbuka misitari hii inayofundisha upatanisho inakuja kupitia kifo cha Yesu msalabani.

- 2 Wakor. 5:19-21, *"Yaani Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu, twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu. Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye."*
- Waru. 5:10, *"Kwa maana tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima."*
- Wakol. 1:20-22, *"Na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa*

yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni. Na ninyi mliokuwa hapo kwanza mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa. Katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu wasio na mawaa wala lawama."

Kwa lugha nyingine, Mungu alimchukua Kristo ambaye hakujua dhambi, kuwakilisha dhambi zetu na kupata adhabu kwa sababu ya dhambi katika kifo chake msalabani, ili kwamba sisi, ambao ni maadui, waliohamishwa kutoka kwa Mungu kwa sababu ya dhambi zetu, ili kwamba tupatanishe kwake Mungu! Na kupitia kifo cha Kristo tuweze kuwa wenye haki wa Mungu katika yeye. 2 Wakor. 5:21, *"Yeye asiyejua dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye."*

Tunaweza tukawa watakatifu, bila mawaa na kusogea mbele ya uso wake ka sababu makosa yetu ni mabaya:

- Wakol. 1: 22, *"Katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake watakatifu wasio na mawaa wala lawama."*
- 2 Wakor. 5:19, *"Yaani Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanishi."*
- Waru. 4:6-8, *"Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo, heri waliosamehewa makosa yao, na waliositiriwa dhambi zao. Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi."*

Hakika, upatanishi unawezekana kwa sababu Mungu amemtoa Yesu kama "*mpatanishi*" kwa ajili ya dhambi zetu!

Neno "*upatanishi*" inaelezea dhabihu iliyoandaliwa kwa ajili ya dhambi. Ilitumika kuelezea dhabihu zile ambazo Mataifa walizitoa kwa miungu yao.

Lakini katika Agano Jipya, ni Mungu ndiye anayetoa "*upatanishi*", siyo mwanadamu!

- 1 Yoh. 2:1-2, *"Watoto wangu wadogo nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiyo kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote."*

- 1 Yoh. 4:10, *"Na hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu."*

Hii inaonyesha upendo mkubwa ambao Mungu anao dhidi yetu, na amefikia wapi katika kumpatanisha mwanadamu ili aweze kumrudia! Ni pale tu tunapoelewa maana na hatua za "*upatanishi*" (sambamba na "*kupatanishwa*") kwamba tunaanza kushukuru wingi wa ajabu wa rehema za Mungu na upendo kwa ajili ya mwanadamu.

Lakini Mungu aliendelea sana kuliko kumtuma mwanaye afe msalabani kama mpatanishi aliyeandaliwa kwa ajili ya kupatanisha mwanadamu amrudie Mungu; pia ameendelea...

Huduma Ya Upatanishi

Mungu aliwatuma "mabalozi"

Zingatia Paulo anasema kwamba Mungu:

- 2 Wakor.5:18, *"Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake Kristo, naye alitupa huduma ya upanisho."*
- 2 Wakor. 5:19, *"Yaani Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho."*

Kuna huduma (kutenda kazi) ambalo katika neno la upatanisho inatakiwa ifahamike kwa wengine pia.

Kimsingi mitume walikuwa na hili "*huduma*". Neno mtume inamaanisha "mtu aliyetumwa". Katika njia ya kipekee walitumwa ili kuhudumu kama "mabalozi" wake Kristo katika ulimwengu! 2 Wakor. 5:20, *"Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu."*

Hivyo basi, kupitia mitume — kupitia neno lao — Mungu anatusihi — Kristo pia anatuonya: "*...mpatanishwe na Mungu!*" (2 Wakor. 5:20).

Kwa hiyo, upendo wa Mungu mkuu umeonyeshwa katika ukweli kwamba yeye naye aliwatuma mabalozi kuwambia ulimwengu kile alichokifanya ili kumpatanisha mwanadamu amrudie yeye.

“Mabalozi” wake leo

“*Huduma ya upatanishi*” bado inaendelea leo kwa sababu watu bado wanapotea katika dhambi zao! Mungu bado anawapenda hao ambao wamepotea; lakini “*mabalozi*” wa Mungu ni wakina nani leo? Ni nani atakayepeleka neno la “*upatanishi*” kwa wengine? Ambao Mungu pamoja na Kristo watawasihi na kuwapatanisha: *“Mpatanishwe na Mungu!”?*

Kama hakutakuwa na mabalozi wa “kutoa maneno katika vinywa vyao” kama mitume walivyokuwa, Kristo bado ana mabalozi wake leo:

Watu wa Mungu wanaotangaza utukufu wake ni mabalozi wake leo. 1 Petr. 2:9-10*, “Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu, ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema.”*

Kuna watu waaminifu, waliofundishwa vizuri ambao pia wanaweza kuwafundisha na wengine. 2 Tim. 2:2*, “Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu, watakaofaa kuwafundisha na wengi.”*

Kwa kweli, Wakristo WOTE wanatakiwa kuhusika katika “*huduma ya upatanishi*”!

Baadhi wanaweza “kwenda”, wakati wengine wanaweza “kutuma”. Waru. 10:14-15, *“Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema!”*

Katika njia yo yote tunayo hudumu, tunatakiwa tukumbuke kwamba tunafanya kazi nzuri katika huduma ya Mungu ya upatanishi leo!

Hitimisho

“*Upatanisho*” ina umuhimu kiasi gani na “*huduma ya upatanisho*”? Kama Mungu ana “tusihi” na Kristo “anatuonya” hakika inatakiwa iwe muhimu, makazi ya milele ya nafsi moja inategemea kama amepatanishwa na Mungu!

Je hii haituhimizi?

- Kwanza kupatanishwa wenyewe?
- Na baadaye kushiriki katika huduma ya upatanisho kwa ajili yaw engine?

Wazo la mwisho: Ukweli kwamba Mungu “anatusihi” na Kristo “anatuonya” ili tupatanishwe anatuambia baadhi ya mambo ambayo ni ya muhimu kwetu kukumbuka..... Upatanisho haina ukomo (lazima tukubali!). upatanisho pia si wa ulimwengu mzima (wengine watapotea!)

Hakika, neema na huruma ya Mungu aliyoitoa kutokana na kifo cha mwanaye isipokelewe bure! Kama Paulo anavyoendelea kusema: Waeb. 5:9,

Je WEWE umepatanishwa kwa Mungu? Ili hiyo itokee mtu ni lazima awe mkristo. Zifuatazo ni hatua mhimu zinazofanya hilo liwezekane:#

- **Imani**. Waeb. 11:6, "*Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu, umri sawa na wa kwangu alikuwa haamini kuwa Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye ana kwa ana kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ili kuwa ni nzuri. Lakini ili kuwa upande ambao ni salama, labda anaweza kwenda kanisani, na kama akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri na kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, “mambo haya hayafanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima umwamini yeye kwa moyo wako wote, la sivyo huwezi kumpendeza.*”

- **Toba.** Matend. 2:38, “*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”* Matend. 11:18, “*...Mungu amewapa pia mataifa toba liletalo uzima.*” Kama ulikuwa una lala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, “kuna mwizi ndani humu!” unachukuwa simu na taratibu unawapigia polisi, ukiwambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani ya nyumba yako. Kidogo, unawasikia wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, “samahani; samahani!” anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadilisha maisha yake ili kwamba asiibe tena. Ni badiliko la akili linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kukifanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Rum. 10:9-10, “*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa*

Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu." Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

Zingatia katika kifungu hapo juu kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekea katika kitu fulani; siyo kwamba tayari mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki inapatikana, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitakakumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa alipanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa mpendwa wangu ninayependezwa naye.*" (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi ya kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia alisema "*imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

  Hakika, tusipobatizwa, bado tupo katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni makabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, ulisema ubatizo ni kwa ajili ya nini? *"Kwa ajili ya ondoleo la dhambi."* Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

  Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. *"Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ukabatizwe uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16).

  Ubatizo ni agizo lililotolewa na Mungu.

  Ubatizo unaitwa maziko. "*Hivyo mnazikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kama vile Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, hivyo na sisi tuenende katika*

upya wa uzima." (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale ni lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaungana kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6).

Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa njia ya ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hapo juu inasema ubatizo ni maziko. Hatuendi makaburini na kuchukua udongo kidogo na kuweka juu ya mwili wa marehemu.

Kama hujafanyika mshiriki wa kanisa la Kristo, kwa nini usizingatie leo"